

# Ngono bila kondomu

Spijo alikuwa na usiku mzuri sana akaishia kufanya vitu ambavyo hakumaanisha kuvifanya, akafanya maumivu ya kichwa yaongezeke zaidi! Angali nini kilichompata kwenye katuni hapo juu. Kama ingekuwa ni wewe ungefanya nini?

Malizia hadithi ya Spijo kwa kutumia utunzi wa hadithi za michoro mtandaoni. Unaweza kushirikisha marafiki zako utunzi wako kwakutumia mtandao wowote wa kijamii unaoupenda.

[\[Katuni za michoro\]](#) [\[Karatasi ya ukweli\]](#) [\[Maelezo ya mwezesaji\]](#)

[>> WhatsApp Download <<](#)

## Maelezo muhimu:

Huna uhakika jinsi ya kuongea na mpenzia wako kuhusu kutumia kondomu? Au kwanini ni muhimu sana? Zifuatazo ni dondoo muhimu:

- Kondomu ni njia moja wapo na pekeeya ya kujilinda na virusi vya ukimwi na magonjwa ya ngono, pia inaweza kuzuia mimba zisizopangwa.
- Kondom zinamotokeo mazuri. Zinaweka vizuizi kimwili kati ya shahawa za mwanaume na uke wa mwanamke. Kondom ya kike huwekwa ndani ya uke kabla ya tendo, wakati kondom Oza kiume huvalishwa nje ya uume.
- Kama unataka kufanya ngono lakini hauna uhakika kuhusu jinsi ya kutumia kondomu basi jifunze, jifunze chukua kondomu na ndizi (ama kifaa chochote kinakachofaa) na jaribu kusalisha kondomu kwa kuipandisha kutokea chini. Kwanjia hiyo utajihisi kujiamini na kuwa tayari wakati ukiwadia.
- Inaweza ikawa rahisi kunogea kwa wakati huo na usitumie kondomu. Kulizungumzia hili na mwenzi wako kabla inamaanisha wote mnauhakika ni kitu gani mnataka.
- Inawezekana usimfahamu vizuri mtu unayepanga naye kufanya naye ngono – utapata kuwafahamu vizuri kwa kuongelea jinsi ya kujilinda na virusi vya ukimwi, na magonjwa ya ngono na mimba zisizo pangwa.
- Ikiwa mwenza wako anakulazimisha kufanya ngono bila kondomu au hakubali kutumia, hii inaweza ikawa ni ishara kwamba upon a mtu ambaye hajitunzi na hakujali wewe vya kutosha.
- Kumbuka kuwa hupaswi kutumia kondomu zaidi ya mara moja, hata kuvaa mbili kwa pamoja, hii hutengeneza msugvano na kondomu inaweza kupasuka
- Kwa kawaida kondomu huja ikiwa imesha lainishwa lakini ukiongeza kilainishi inapunguza hatari ya kupata maambukizi ya virusi vya ukimwi na huleta raha. Kama unatumia kindomu ya mpira hakikisha unatumia kilainishi cha maji kwa kua kilainishi cha mafuta huweza kusababisha kondomu kupasuka.

## Mawazo ya mjadala:

Unafikiria nini kuhusu kufanya ngono kwa kutumia kondomu na bila kondomu? Inawezekana kua hujawahi kulifikiria hili mwanzo, sasa unafikiri nini kuhusu kufanya ngono bila kondomu?

- Ni nini mtazamo wa marafiki, wazazi na jamii yako kwa ujumla kuhusu kondomu? Kwanini unadhani watu wanaizungumzia vibaya au vizuri?
- Kuna mila zozote, mitazamo au sababu yoyote iliyopo inayozuia vijana kutumia kondomu mahali unapoishi?
- Unafikiri ni sababu gani zinazo fanya wanaume wasitake kutumia kondomu? Na wanawake?
- Unadhani kunahatari gani za kuto kutumia kondomu? Je kuna faida yeyote?
- Unafikiri ni wakati gani ambao kuna uwezekano mkubwa wa vijana kufanya ngono bila kondomu?
- Je nisahihi kubeba kondomu wakati unapo toka? Kwanini? Na kwanini sisahihi?

*Young Voices Africa ni kikundi kinacho jadili kuhusu mjadala mbalimbali ya afya ya uzazi na kufanya ngono salama. Kimekuwa kikiendelezwa na vijana na nikwaajili ya vijana kuanzi miaka 15 mpaka 24 nchini Afrika ya kusini.*

Last full review:

23 February 2021

Next full review:

23 February 2022